

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI
JESHI LA ZIMAMOTO NA UOKOAJI**



TANGAZO LA NAFASI ZA AJIRA

Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji anatangaza nafasi za ajira kwa vijana waliohitimu mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) au walioko kambini wenye sifa zifuatazo: -

1. Wenye elimu ya kidato cha Nne

- (i) Waliohitimu kidato cha nne kuanzia mwaka 2020 na 2021.
- (ii) Umri kuanzia miaka 18 hadi 23

2. Sifa za mwombaji

- (i) Awe raia wa Tanzania kwa kuzaliwa.
- (ii) Awe amehitimu mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) au aliyepo kambini ya JKT.
- (iii) Awe na cheti cha kuzaliwa.
- (iv) Awe na Kitambulisho cha Taifa au Namba ya Utambulisho iliyotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho. (NIDA)
- (v) Awe na afya njema ya kimwili na kiakili.
- (vi) Asiwe na Kumbukumbu za Uhalifu.
- (vii) Awe hajaoa au kuolewa.
- (viii) Asiwe na alama za kuchorwa mwilini (Tatoo).
- (ix) Awe hajawahi kutumia aina yoyote ya madawa ya kulevya.
- (x) Awe tayari kuhudhuria mafunzo ya taaluma ya Zimamoto na Uokoaji.
- (xi) Awe hajawahi kuajiriwa serikalini.
- (xii) Awe mwenye urefu usiopungua futi 5.7 kwa mwanaume na futi 5.4 kwa mwanamke.
- (xiii) Awe tayari kujigharamia katika hatua zote za usaili endapo ataitwa.

3. Utaratibu wa Kutuma Maombi


- (i) Barua za maombi ziandikwe na mwombaji kwa mkono zikiambatishwa na nakala zifuatazo; -
- (a) Nakala ya cheti cha kuzaliwa.
 - (b) Fomu ya uthibitisho wa siha njema kutoka kwa mganga wa serikali.
 - (c) Nakala ya Kitambulisho cha Taifa au namba ya NIDA.
 - (d) Nakala ya cheti cha kufuzu mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT)
 - (e) Picha tatu za Pasipoti.
 - (f) Nakala ya cheti cha Kidato cha Nne kinachotambulika na mamlaka za elimu nchini.
 - (g) Barua ya Utambulisho kutoka kwa afisa mtendaji wa Kijiji/mtaa

NB: Nakala za vyeti zithibitishwe na Kamishna wa viapo au Hakimumu.

- (i) Waombaji waelekeze maombi yao moja kwa moja kwa: -

**Kamishna Jenerali,
Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Makao Makuu,
1 Mtaa wa Zimamoto,
S.L.P. 1509,
41102 VIWANDANI,
DODOMA.**

- (ii) Barua zitakazowasilishwa mkononi **hazitapokelewa.**
- (iii) Waombaji wote waandike namba za simu kwenye barua zao za maombi.
- (iv) Mwombaji atakayewasilisha nyaraka za kughushi au taarifa za uongo atachukuliwa hatua za kisheria.
- (v) Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **08 Disemba, 2022.**


M. S. Semwanza, *ndc*

**KAMISHNA
Kny. KAMISHNA JENERALI
JESHI LA ZIMAMOTO NA UOKOAJI
24 Novemba, 2022**